


# MANIFESTO YA WAKAAJI WA MUKURU

KWA REUBEN | KWA NJENGA | VIWANDANI



"Ni matumaini yetu kuwa manifesto hii itakuwa **kama makubaliano kati yako kama mgombea uchaguzi na watu wa Mukuru** na itakuwa kwenye kitovu cha miradi yote ya maendeleo itakayotekelezwa katika wadi zetu 4, kwa miaka mitano ijayo."

## Utangulizi

Sisi, wakazi wa wadi za Mukuru kwa Reuben, Mukuru kwa Njenga, Viwandani na Imara Daima katika maeneobunge ya Embakasi Kusini na Makadara tumetayarisha manifesto hii kama nyenzo ya kutuwezesha kusema kwa sauti moja ili kutafuta suluhisho kwa matatizo tunayokabiliana nayo.

Ni matumaini yetu kuwa manifesto hii itakuwa kama makubaliano kati yako kama mgombeauchaguzi na watu wa Mukuru na itakuwa kwenye kitovu cha miradi yote ya maendeleo itakayotekelezwa katika wadi zetu 4, kwa miaka mitano ijayo.

## Chanzo

Matamanio ya wananchi yanayotetewa katika Manifesto yetu yanatokana na matakwa yetu ambayo yameangaziwa katika Ruwaza ya Mukuru kama Eneo Maalum Kwa Maendeleo Kimajengo (**Mukuru SPA**). Mnamo Agosti 11, 2017, serikali ya Kaunti ya Nairobi iliorodhesha mitaa ya Mukuru kwa Njenga, Kwa Reuben na Viwandani kwenye gazeti rasmi la serikali kama maeneo ya Mipango Mahsusi kupitia Notisi nambari 7654.

Kama ilivyotazamiwa baada ya azimio hilo, mradi wa Mukuru SPA uliundwa kwa kuwashirikisha kikamilifu wananchi katika sekta zilizotambuliwa kuwa nguzo muhimu katika mchakato wa mipango ya sekta mbali mbali.

- Elimu, Vijana na Utamaduni
- Huduma za Afya
- Mazingira na Mali Asili
- Nyumba, Miundomsingi na Biashara
- Ardhi na Miundo ya Taasisi
- Fulusi na Maendeleo ya Kiuchumi
- Maji, Usafi na Nishati; na
- Uletaji Pamoja wa Jamii, Mawasiliano na Uratibu

Mpango ulioundwa unaweza kuamili kama mwongozo muhimu katika kuyasuluhisha matatizo yanayoangaziwa katika Manifesto hii.

## Tatizo

Mitaa mitatu ya Mukuru kwa Njenga, Kwa Reuben, na Viwandani ni makao kwa watu wapatao 400,000. Wengi wetu, tunaoishi katika maeneo haya, tulitoka kwetu vijijini na kuja mjini na matumaini ya kupata kazi na Maisha bora kwetu na kwa familia zetu.

Baadhi yetu wamefanikiwa lakini kwa kuwa wengi wetu hawana ujuzi wa kikazi na wana viwango vya chini vya elimu, wamebaki bila kazi.

Makaazi haya yana matatizo mengine mengi. Matatizo haya ni pamoja na ukosefu wa mpango wa kuzoa taka, na kusababisha nyingi ya takataka mitaani mwetu kutupwa kwenye Mto Ngong' ulioko karibu; shule duni, ukosefu wa ajira, umasikini na uhaba wa maji na miundo ya kudumisha usafi; na yanahitaji suluhu ya dharura.

Hata hivyo, tatizo ambalo ni la kukandamiza na kuogofya kwetu ni hofu tunayoishi nayo daima ya kufurushwa kwenye ardhi na makazi yetu.

## WITO WA KUCHUKULIWA KWA HATUA

Kama Suluhu, sisi, wakazi wa wadi za Mukuru kwa Reuben, Mukuru kwa Njenga, Viwandani na Imara Daima katika maeneobunge ya Embakasi Kusini na Makadara, tungependa kuona kuwa MATATIZO yafuatayo yanashughulikiwa:

### Mukuru SPA

Wingi wa matatizo katika eneo la Mukuru ulipelekea eneo hili kutangazwa kuwa Eneo Maalum kwa Mipango (SPA) na mpango wa miaka 10 ulioongozwa na wananchi ukaundwa. Mpango huu ulijumuishwa kwenye Mpango Mkuu wa Kaunti ya Nairobi na kujumuishwa kwenye Ruwaza ya Maendeleo ya Jiji la Nairobi. Tunasikitika kuona kuwa mpango wetu haujaidhinishwa na Bunge ya Kaunti ya Nairobi.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba, wewe kama mtarajiwa wetu:

i. **Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA):**

- Kuwasilisha Ruwaza ya Mukuru SPA katika Bunge ya Kaunti ya

Nairobi na kuiunga mkono ili kupitishwa, kuidhinishwa na kutekelezwa.

- Kuwa, utawashawishi wabunge wenzako kuunga mkono uidhinishwaji na upitishaji wa ruwaza hii ya eneo letu.
- Kufanya kazi kwa karibu na kamati ya Bajeti ya Bunge Pamoja na Kamati zingine muafaka kuhakikisha kupewa migao tosha ya bajeti.

ii. **Gavana:**

- Kutoa kipaumbele kwa utekelezaji wa Ruwaza ya Mukuru SPA kaitka Ruwaza Pana ya Kaunti.
- Kutenga rasilimali – nguvukazi na fedha, ambayo itawezesha utekelezaji wa ruwaza ya Mukuru SPA.

iii. **Mbunge (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kufuatilia na kuunga mkno, uidhinishaji na utekelezaji wa ruwaza ya Mukuru SPA.
- Kuhakikisha kuwa kuna nyongeza za rasilimali za ziada zinazohitajika kwa ruwaza ya Mukuru SPA kutekelezwa kikamilifu.

## Elimu

Elimu ni haki ya kimsingi ya binadamu na hutuwezesha sote kufikia uwezo wetu kamili kama binadamu. Haki ya kupata elimu ya bure na lazima ni mojawapo ya haki ambazo sisi kama watu wa Mukuru, tunafaa kupokea. Licha ya hayo, eneo letu, ambalo lina idadi ya wanafunzi wapatao 122,000 lina shule za umma 6 tu.

Idadi hii ya shule za serikali ipo katika eneo lenye shule 182 ambazo hazijasajiliwa wala kufanyiwa udhibiti wa namna yoyote, na zilizo katika hali mbovu ya ukarabati, huku zikiwa na viwango duni vya elimu. Jambo ambalo linatuguza pia ni ugavi wa misaada ya elimu ambao unafanywa kwa njia isiyozingatia haki kwa kuwa haifikii wanafunzi kutoka jamaa hohehahe.

Hali ya kukosa kufikia elimu ya kimsingi ya bure kwa wote miongoni mwa vijana wetu chipukizi ina maana kwamba sisi, hohehahe wa jiji hili, tunakabiliwa na tishio la kukwama kwenye umasikini wa kizazi hadi kizazi.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

i. **Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA), Mbunge wa Bunge ya Taifa (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kuhakikisha ya kwamba NG-CDF, fedha za kaunti pamoja na fedha zingine za serikali ambazo zinatumika katika mpango wa kutoa elimu ya bure ya kimsingi zinaongezwa na kuwafikia wale wanaohitaji zaidi na wale wanaostahili zaidi ili kuwasaidia kujiunga na shule za sekondari, vyuo vya masomo anuwai, na elimu ya juu kwa watoto wetu.
- Kuhakikisha kuwa kuna Usawa wa Kijinsia na haki kwa watu wanaoishi na ulemavu katika shule zote na vilevile kupitia kujengwa kwa shule za watu wenye mahitaji maalum.

ii. **Gavana, Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA), Mbunge wa Bunge ya Taifa (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutoa ahadi ya dhati kuwa utafanya kazi pamoja nasi ili kutenga ardhi ya kujenga chekechea na shule za vidudu katika eneo letu;

iii. **Gavana, Mbunge wa Bunge ya Kaunti:**

- Kutoa ahadi ya dhati kuwa utatenga fedha za kutosha, kwa kuwaajiri walimu, na kununua vifaa vya kufundishia, kuendesha miradi ya chakula na uendeshaji jumla wa chekechea na shule zetu za elimu ya vidudu.

iv. **Gavana, Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA), Mbunge wa Bunge ya Taifa (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kushinikiza ugavi wa rasilimali kutoka kwenye Hazina ya Uswazishaji na kutoka vyanzo vingine vilivyopo, kwa ujenzi wa angalau shule 10 za umma ambazo zitashirikisha shule za msingi, za upili na vyuo vya masomo anuwai.

v. **Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA), Mbunge wa Bunge ya**

**Taifa (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutoa ahadi ya dhati kuwa utatenga fedha za kutosha, kwa kuwaajiri walimu, na kununua vifaa vya kufundishia, kuendesha miradi ya chakula na uendeshaji jumla wa chekechea na shule zetu za elimu ya vidudu.

**vi. Mbunge (hasa wa Bunge ya Taifa):**

- Kutumia hazina ya NG-CDF kwa ujenzi wa madarasa na majiko kwa minajili ya mradi wa chakula shuleni katika eneo la Mukuru.

**vii. Mbunge wa Bunge ya Kaunti, Mbunge wa Bunge ya Taifa (Bunge ya Taifa &Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutoa wito kwa Wizara ya Taifa ya Uchukuzi na Miundomsingi kutenga sehemu ya ardhi ya idara ya utabiri wa hali ya hewa katika eneo la Mukuru kwa minajili ya kuwapa makazi wakazi wote watakaohamishwa kutokana na ujenzi wa shule na miundomsingi mingine katika eneo hili.

## Usafi

Ni 1% tu ya wakazi wa Mukuru ambao wana vyoo vya kibinafsi majumbani mwao, huku nyumba 547 kwa wastani zikishiriki choo kimoja cha umma. Ni vyoo vya mashimo vinavyopatikana zaidi katika eneo letu, lakini havitunzwi vizuri, havivutwi mara kwa mara na huwa vinafurika kila wakati, hasa wakati wa msimu wa mvua. Kinyesi ghafi cha binadamu ambacho huvutwa kutoka vyoo hivi aghalabu humwagwa katika Mto Ngong.

Ukosefu wa sitara, usafi na jinsi ya kudhibiti taka huufanya uhaba wa vyoo kuwa mojawapo ya matishio makubwa kwa afya ya binadamu, hasa kwa kina mama na watoto wa kike, hapa Mukuru.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

**i. Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA), Gavana:**

- Kutoa ahadi ya dhati kuwa utatenga rasilimali muafaka za kifedha na nguvukazi kuhakikisha kuwa mabomba ya kupitisha taka ya choo yanajengwa ili kila ploti iweze

kuunganishwa kwenye mtandao wa mabomba ya taka ya choo.

- Kutoa ahadi ya dhati kwamba utafanya kazi bega kwa bega nasi ili kuunda mfumo wa kudhibiti taka ambao utawapa kandarasi vijana mitaani mwetu ambao watazoa na kuirejeleza taka kote katika mitaa yetu. Jambo hili halitashughulikia tu tatizo la udhibiti wa takataka mitaani mwetu bali pia litashughulikia tatizo la ajira kwa vijana wetu.

## Maji

Sisi hapa Mukuru hununua Takriban mitungi mitatu ya Lita 20 ya maji kwa kila nyumba kila siku, kwa gharama ya shilingi 5-20 kwa kila mtungi.

Hata hivyo, wakazi wengine wa jiji hulipa kiasi kisichobadilika cha shilingi 206 kwa matumizi ya mita 0-6 mchemraba za maji. Kwa hivyo, sisi hulipa 250% zaidi, kwa kila mita moja mchemraba ya maji duni zaidi, kulinganishwa na wakazi wengine wa jiji.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

i. **Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA), Gavana:**

- Kuhakikisha ya kwamba rasilimali zinatengwa kwa ujenzi wa miundomsingi mwafaka ya kuhakikisha kuwa angalau PDD moja inatolewa kwa kila nyumba 50.

ii. **Mbunge (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kufanya juhudi za kuhakikisha kutengwa kwa rasilimali kutoka hazina ya usawazishaji na kutoka vyanzo vingine, kujenga miundomsingi ya maji katika makazi yetu;

## Umeme

Sisi katika mtaa wa Mukuru hatuna maji salama, ya kutegemewa na umeme tunaoweza kumudu bei. Kutokana na hayo, imetulazimu kutegemea wagavi chwara wa umeme ambao wanatutoza bei ya juu kwa kutufanyia uunganishaji hatari ambao mara nyingi

husababisha moto na kukatiza huduma za nguvu za umeme.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

i. **Mbunge (Bunge ya Taifa &Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kufanya kazi bega kwa bega nasi ili kusambaza umeme salama, kwa bei nafuu na wa kutegemewa kwa kila nyumba katika eneo letu.

## Afya

Tunafurahi kuwa serikali yetu ya sasa imejenga vituo vya afya vya kutosha katika eneo letu, kimoja Kwa Njenga, kimoja Viwandani na kingine Kwa Reuben. Lakini tunasikitika kuwa mara kwa mara vituo hivi huwa havina madawa pamoja na vifaa vingine vinavyohitajika ili kufanya kazi inavyofaa.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

i. **Mbunge (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutoa ahadi ya dhati kwamba utaboresha upatikanaji wa huduma chini ya mpango wa Hazina ya Taifa ya Afya (NHIF) ili kuweza kutoa huduma za afya za viwango vya juu kwa wote.

ii. **MCA na Gavana:**

- Kutoa ahadi ya dhati kuwa kutakuwa na madaktari, wauguzi na wahudumu wengine wa kiafya, watakaoweza kuhudumu na kutuwezesha kunufaika na huduma bora za kiafya.

iii. **MCA:**

- Kutuhakikishia kuwa atakuwa mwangalifu wa kufuatilia na kutathmini huduma katika sekta ya afya kwa kuwa kwa mapana huduma za afya zimegatuliwa.

iv. **Gavana na MCA:**

- Kutoa ahadi ya dhati kuwa utafanya kazi pamoja na Mamlaka ya Ugavi wa Vifaa Vya Afya nchini (KEMSA) ili kuhakikisha ya kwamba kuna madawa na vifaa vingine vya kiafya katika hospitali zetu.

- Kutoa ahadi ya dhati kuwa kutakuwa na ambalanzi katika kila wadi ili kuhudumia wanaohitaji matibabu ya dharura.

## Ardhi

Tumechoka na kupokea notisi za kufurushwa, kuhamishwa kutoka makazi yetu, na kubomolewa kwa maeneo ya biashara na makazi na maisha yetu kuharibiwa.

Tunaelewa kuwa karibu eneo zima la ardhi ya Mukuru Kwa Njenga, Kwa Reuben na Viwandani lilikuwa ardhi ya umma ambayo iligawanywa na serikali kuwa ploti na kupewa watu binafsi kwa ujenzi wa viwanda vidogovidogo.

Watu na kampuni zilizopewa ploti hizi walipewa hati za kumiliki ambazo zilikuwa na masharti maalum. Mojawapo ya masharti haya ilikuwa ni kuwahitaji kuzistawisha katika muda wa miaka miwili baada ya wao kupewa. Ikiwa hawangefanya hivyo, serikali ilipewa mamlaka ya kuzibatilisha hati hizi.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

i. **Mbunge (Bunge ya Taifa &Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutoa ahadi ya dhati kushinikiza Tume Ya Ardhi pamoja na Wizara ya Ardhi kuifanya ardhi katika eneo la Mukuru kutangazwa kama ardhi ya umma ili kuwezesha miradi ya maendeleo kustawishwa katika eneo letu.

## Umasikini na Ukosefu wa Ajira

Umasikini umekita mizizi katika jumuia yetu na hunasibishwa hasa na ukosefu wa ajira na fursa za elimu. Wengi miongoni mwetu wanafanya kazi kama vibarua katika viwanda vilivyoko karibu na makazi yetu huku wengine wakiendesha biashara ndogondogo. Mapato yetu ni duni na yasiyoweza kutuwezesha kulisha familia zetu.

Changamoto zetu kuu ni nafasi chache za ajira, ukosefu wa mtaji, masoko na nafasi za kuendeshea biashara ambazo zina fifaa na

huduma zinazostahili; mambo ambayo huwasukuma wengi wetu kutafuta kazi za kibarua zenye malipo duni. Tunasikitishwa pia na maslahi ya wazee na makundi mengine ya wanyonge ambayo hayana msaada.

Linalotutia wasiwasi mwingi hasa ni hali iliyotanda ya ukosefu wa matumaini miongoni mwa vijana wetu, jambo ambalo limewasukuma kuingilia mienendo hatari kama vile matumizi ya mihadarati na uhalifu.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

i. **Mbunge (Bunge ya Taifa & Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutoa ahadi ya dhati kushinikiza Serikali ya Taifa na Serikali ya Kaunti kutenga fedha kupitia hazina ya CDF na fedha zingine za serikali ili kuunda Mifumo ya Ulinzi wa Kijamii kulinda wakongwe na makundi mengine ya wanyonge.

ii. **Mbunge wa Bunge ya Kaunti (MCA), Gavana:**

- Kutetea uwepo wa nafasi zaidi katika viwanda vya eneo letu ambapo wakazi wa eneo hili wanaweza kuajiriwa.

iii. **MCA, Gavana na Mbunge (Bunge ya Taifa &Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutumia fedha zinazotengwa na serikali kwa minajili ya kuunda nafasi za watu kujiajiri wenyewe (Sekta ya Jua Kali), biashara ndogondogo na mipango ya mikopo kwa wanabiashara ili kusaidia ajira.

iv. **MCA, Gavana:**

- Kutenga fedha zinazohitajika pamoja na rasilimali kwa ujenzi wa angalau masoko matatu mapya na yenye kupokea huduma bora katika eneo letu.

v. **Gavana, Mbunge (Bunge ya Taifa &Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutenga pesa kupitia mpango wa NG-CDF na fedha zingine za serikali kujenga nyenzo za kuwasaidia wakongwe na makundi mengine ya wanyonge.

## Uongozi

Maeneo haya matatu yalipotangzwa kuwa Maeneo ya Mipango Maalum, shughuli za maendeleo zaidi zilisitishwa kwenye mitaa hii yote hadi kukamilika na kuundwa kwa mpango utakaowashirikisha wananchi. Mpango ambao uliongozwa na wananchi uliundwa katika muda uliohitajika.

Mpango huu ulitoa fursa adimu kwa wananchi kuathiri miundo na utekelezaji wa mipango ya vitongojiduni si katika kaunti hii tu, bali kote nchini pia. Dhana kubwa hapa ilizunguka swala la jinsi "wakaazi wa vitongoji duni wanavyowekwa kwenye kitovu cha mipango."

Kwa hivyo, azimio hili lilikuwa fursa ya kuunda, kuboresha na kutoa kielelezo, kwenye kiwango cha jiji, picha kamili ya maana ya dhana ya kuweka wanajamii kwenye kitovu cha mipango.

Hili lilitekelezwa vizuri sana na likazaa ruwaza ya Mukuru SPA. Ni kwa kuzingatia haya ambapo wakazi wa Mukuru wangependa kutafuta ushirikishwaji na uwakilishwaji zaidi kwenye majukwaa mbali mbali yanayonuia kusaidia katika masuala ya utoaji wa huduma.

**Tunachotaka:**

Tunakuomba kama mtarajiwa:

i. **MCA, Gavana na Mbunge (Bunge ya Taifa &Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

- Kutoa ahadi ya dhati kwamba mwanachama wa Kundi/ Kamati Tekelezi ya Mukuru SPA atapata nafasi ya kuhudumu katika Kamati ya Maendeleo ya Wadi, hazina ya NG-CDF na kamati zingine za mipango na maendeleo.

ii. **Mbunge wa Bunge ya Kaunti, Gavana, Mbunge (Bunge ya Taifa &Seneti) na Mwakilishi wa Kina Mama katika Bunge ya Taifa:**

Kutoa ahadi ya dhati kufanya kazi bega kwa bega na Kamati Tekelezi ya Mukuru SPA ili kuchangia katika michakato muhimu ya kaunti kama vile uundaji wa Bajeti ya Kaunti, kufanya marudio ya mipango na mikakati ya maendeleo ya kaunti.

**Mimi,...........................................................................................kwa**

**unyenyekevu nikiomba kuchaguliwa kama ..................................**

**...............................................................................katika Uchaguzi Mkuu wa Agosti 9, 2022 NINATANGAZA WAZI kwa moyo wangu wote kuunga mkono MANIFESTO YA JAMII iliyoundwa na wananchi wa wadi za** Mukuru kwa Reuben, Mukuru Kwa Njenga, Viwandani na Imara Daima katika maeneobunge ya Embakasi na Makadara. **Ninaaahidi pia kuunga mkono na kufanya bidii ili kuhakikisha kutekelezwa na kuafikia kwa malengo yote yaliyoangaziwa katika MANIFESTO YA JAMII punde tu nitakapochaguliwa katika nafasi hii ninayowania.**

**Mgombeaji:**

**Sahihi: ..................................................................................................**

**Tarehe: .................................................................................................**

**Shahidi:** Mkazi wa Mukuru SPA:

**Sahihi: ..................................................................................................**

**Tarehe: .................................................................................................**

**Shahidi:** Mwanachama wa Kundi/ Kamati Tekelezi ya Mukuru SPA

**Sahihi: ..................................................................................................**

**Tarehe: .................................................................................................**

## NOTES




# MUKURU PEOPLE'S MANIFESTO

KWA REUBEN | KWA NJENGA | VIWANDANI

## Introduction

We, the people of Mukuru Kwa Rueben, Mukuru Kwa Njenga, Viwandani and Imara Daima Wards of the Embakasi South and Makadara Constituencies, have prepared this manifesto as a rallying- point to speak in one voice and advocate for solutions to the challenges that we face.

It is our hope that our manifesto will act as an agreement between you, as an aspiring candidate and us the people of Mukuru and that it will be at the heart of all development programs undertaken in our 4-Wards, for the next five years.

## Background

The people's aspirations championed in our Manifesto are informed by the needs captured in the **Mukuru Special Planning Area** (SPA) Local Development Plan. On 11th August, 2017, the County Government of Nairobi declared the informal settlements of Mukuru Kwa Njenga, Kwa Reuben and Viwandani as Special Planning Area through a Gazette Notice No. 7654.

As envisaged after the declaration, the Mukuru SPA plan was developed with us, the residents, playing an active role in the key sectors identified as the most critical pillars in the sectoral planning process. The eight sectors were:

- Education, Youth and Culture
- Health Services
- Environment and Natural Resources
- Housing, Infrastructure and Commerce
- Land and Institutional Framework
- Finance and Economic Development
- Water, Sanitation and Energy; and
- Community Mobilization, Communication and Coordination

We, the people of Mukuru, are persuaded that the Mukuru Integrated Development Plan (MIDP) is an important guide in solving the issues raised in this Manifesto.

**Statement of the problem**

The three settlements of Mukuru Kwa Njenga, Kwa Reuben, and Viwandani are home to about 400,000 people. Most of us, who live in these settlements, left our rural homes and come to the city with the hope of finding work and better lives for ourselves and our families. Some of us were successful but many of us being unskilled remain jobless.

Our settlements have many problems; we have no waste collection and most of the garbage in our area is dumped into the nearby Ngong' River. The problems of poor schools, unemployment, poverty and the lack of adequate water and sanitation services are pressing and need urgent action. However, the constant threat of eviction from our land and homes is certainly our most terrifying worry.

**CALL TO ACTION**

We, the people of Mukuru Kwa Rueben, Mukuru Kwa Njenga, Viwandani and Imara Daima Wards of the Embakasi South and Makadara Constituencies, would like to see that the following CONCERNS are adequately addressed:

## The Mukuru SPA

The countless problems we face in Mukuru led to the area being declared as a Special Planning Area (SPA) by Nairobi City County Government. A10-year, citizen-led, plan has now been developed.

However, we are saddened to note that our plan has not been approved by the Nairobi City County Assembly.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

i. **Member of the County Assembly (MCA);**

- To support the passing, approval and implementation of the Mukuru SPA plan.
- To lobby other members of the assembly to support the approval and passing of this development Plan for our area.
- To work closely with the Assembly's Budget and other related Committees to ensure

adequate budgetary allocations for plan implementation.

ii. **The Governor**

- To table the Mukuru SPA Plan before the Nairobi City County Assembly for its passing, approval and implementation.
- To mainstream and prioritize the implementation of the Mukuru SPA Plan in the County's Integrated Development Plan.
- To allocate the necessary resources- human and financial, that will help in the implementation of the Mukuru SPA Plan.

iii. **Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the County Woman Representative in the National Assembly**

- To monitor and support the passing, approval and implementation of the Mukuru SPA Plan.
- To ensure that the necessary additional resources are provided for the full implementation of the Plan.

## Education

Education is a basic human right and helps us all realize our human potential. The right to free and compulsory education is one which, we the people of Mukuru, should be able to access. Yet our area, that has a school going population of about 122,000, is served by only 6 public schools.

This number of public schools is against a total of 182 unregistered and unregulated education facilities that are dilapidated and often provide very poor education.

Of concern to us is, also the unfair distribution of bursaries that often do not reach the poorest. The failure to make provision for universal free basic education for our young and vibrant population means that we, the city's poorest, are faced with the real threat of inter-generational poverty.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

**i. Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the County Woman Representative in the National Assembly:**

- To push for the allocation of resources from the Equalization Fund and from any other sources available, for the construction of at least 10 public schools that include primary, secondary and TVET facilities.
- To push for the allocation of resources from the Equalization Fund and from any other sources, for the hiring of teaching staff, the purchase of learning materials, the running of school feeding programs and the general upkeep of our primary, secondary and TVET facilities.

**ii. Member of the National Assembly:**

- to use our NG-CDF for the construction of classrooms and kitchens to support school feeding programs in all schools in Mukuru.

**iii. The Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate), the County Woman Representative in the National Assembly and Member of the County Assembly:**

- To lobby the National Ministry of Transport and Infrastructure to designate a space within the Mukuru SPA decanting site on the Metrological land for the re-settlement of all those households that are likely to be displaced by the development of public schools and any other infrastructure development.
- To make a commitment to work closely with us to identify land for the construction of enough day care and early childhood centers in our area.

**iv. The Governor, Member of the County Assembly:**

- To make a commitment to allocate the necessary financial resources, for the hiring of teaching staff, the purchase of learning materials, the running of feeding programs and the general upkeep of our day care and early childhood education centers.

v. **Member of Parliament (the National Assembly & Senate), the County Woman Representative in the National Assembly and Member of the County Assembly:**

- To ensure that NG-CDF, County and all other government funds that support free basic and higher education through the provision of education bursaries are increased and reach the neediest and most deserving to encourage entry into secondary, TVET, and higher education for our children.
- To ensure Gender Equality and the rights of persons living with disabilities are catered for in all schools and also through the development of special needs schools.

## Sanitation

Only 1% of residents in Mukuru have access to private, in-home toilets with an average of 547 households sharing one public toilet. Pit latrines are the most common type of toilet in our area, but are improperly maintained, are not regularly emptied and often overflow, particularly during the rainy seasons. The raw human waste exhausted from these latrines is usually emptied directly into the Ngong River.

The lack of privacy, hygiene and waste treatment make inadequate toilets one of our greatest threats to human health, especially for women and girls, in Mukuru.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

i. **Member of the County Assembly (MCA), Governor:**

- To make a commitment that you will allocate the necessary human and financial resources to ensure the necessary trunk and lateral sewers are built so that every plot can be connected to the sewer;
- To make a commitment that you will work closely with us to set up a waste management system that contracts our youth groups in every village to collect and recycle waste in our settlements. This will not only help cure the important

question of waste management but also help address the issues of youth employment.

## Water

We, in Mukuru purchase about three 20-liter containers of water per household in a day at a cost of KES 5-20 per jerry can. This amount is roughly 1.8 cubic meters per month at a cost of KES 1,050. Yet other city residents pay a flat rate of KES 206 for consumption of 0-6 cubic meters of water.

We, therefore, pay 250% more, per cubic meter for poorer quality water, than other city residents.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

i. **Governor, Member of the County Assembly (MCA):**

- To ensure that resources are allocated for the construction of the necessary infrastructure to ensure that at least one PPD is provided for every 50 households.

ii. **Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the Woman Representative in the National Assembly**

- To push for the allocation of resources from the equalization fund and from any other sources, to develop the necessary water infrastructure in all our settlements.

## Electricity

We, in Mukuru, do not have safe, reliable and affordable electricity. Because of this we are often forced to rely on informal electricity suppliers who charge us highly for dangerous connections often leading to fire outbreaks and constant blackouts.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

iii. **Member of the County Assembly (MCA), Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the County Woman Representative in the National Assembly:**

- To work with us to provide every household in our area with safe, affordable and reliable electricity.

## Health

The people of Mukuru are happy that the current government administration has constructed sufficient health centres in our area, one in Kwa Njenga, one in Viwandani and the other in Kwa Rueben. We however note that these centres often run out of medicine and the protective gear required to operate properly.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

i. **Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate), the County Woman Representative in the National Assembly and Member of the County Assembly (MCA):**

- To make a commitment that you will Improve accessibility, availability, and affordability of the National Hospital Insurance Fund to deliver high quality health care services to all.

ii. **MCA and Governor:**

- To make a commitment to deploy more doctors, nurses and other health personnel, to provide care and enable us benefit from proper health services.

iii. **Gavana and MCA**

- To make a commitment to work with the Kenya Medical Supplies Authority (KEMSA) to ensure there are drugs and medical supplies in our hospitals.
- To make a commitment that you will ensure that there is an ambulance in every ward to support medical emergencies.

## Land

The people of Mukuru, are tired of receiving eviction notices, of being evicted from our area, of having our homes demolished and our businesses and livelihoods destroyed. We are aware that almost all the land in Mukuru Kwa Njenga, Kwa Reuben and

Viwandani was public land that was divided into plots and allocated by the state to individuals and companies for the development of light industries.

The people and companies who received these plots were given titles that had special conditions. One condition was that they should develop their plots within a period of two years after allocation. In the event that they did not develop the land, the government was given the power to cancel the titles. The government has failed to take back the land putting us at great risk of forced evictions.

Recently about 15,000 households were forcefully evicted from their homes and had their property, schools and other amenities demolished. This is despite having an Evictions and Resettlement Procedures Bill which was introduced in Parliament in 2012 by Shabbir Shakeel but was however never passed.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

i. **Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the County Woman Representative in the National Assembly:**

- To make a commitment to push for the National Land Commission and the Ministry of Land to have the land in Mukuru declared as public land to enable proper upgrading in our area.
- To lobby together with MPs in other informal settlements to revive and pass the Evictions and Resettlement Bill.

## Youth and Unemployment

Poverty is widespread in our community and is often linked to lack of employment and educational opportunities. Many in our area, work as casual laborers in the manufacturing industries situated close to our settlements while others operate small-scale businesses. Our earnings are often low and inadequate to feed our families.

Of concern to us are the minimal employment opportunities, the lack of capital, markets and trading spaces with adequate services, that lead many of us to seek low paying jobs as casuals.

We are also concerned by the welfare of the elderly and other vulnerable groups that do not have enough support. Of great worry to us is the widespread lack of hope especially amongst our youth, which has driven them to engage in high-risk activities such as drug abuse and crime.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

i. **Member of the County Assembly (MCA), Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the County Woman Representative in the National Assembly:**

- To make a commitment to push both the National and County Governments to allocate funds through the CDF and all other governmental funds to progressively develop Social Protection Systems to support the elderly and other vulnerable groups.
- To establish 3 ICT Innovation Hubs one for each settlement to support youth training and employment.

i. **Governor, Member of the County Assembly (MCA):**

- To lobby for more slots in the Local Industries where our residents can be employed.

ii. **Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate), the County Woman Representative in the National Assembly and MCA:**

- To lobby for governmental funds directed towards supporting the Jua Kali Sector, micro enterprises and credit schemes to create employment in Mukuru.

iii. **MCA, Governor:**

- To allocate the necessary funds and resources for the construction of at least three new serviced markets in our area.

## Governance

When the 3 informal settlements of Mukuru were declared as a Special Planning Area, a citizen-led planning process was initiated. The most important aspect of the planning process, was how the people of Mukuru and other stakeholders were placed at the center of planning.

It is with this in mind, that the citizens of Mukuru would like to seek further involvement and representation in the various platforms set to address developmental issues and service delivery.

**What we are asking:**

We, ask you as our potential:

i. **Member of the County Assembly (MCA), Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the County Woman Representative in the National Assembly:**

- To make a commitment that a member of the Mukuru SPA Working Group/Committee shall get a place in the Ward development committee, the NG-CDF and other various development and planning committees.

ii. **Member of the County Assembly, Governor, Member of Parliament (the National Assembly & Senate) and the County Woman Representative:**

To make a commitment to work with the Mukuru SPA Working/Committee to make input in key processes like the county budgeting, reviewing of development plans and strategies.

**I, ......................................................................................................**

**humbly seeking to be elected as .......................................................................**

**................................................................................ in the coming General Election in August 9, 2022 HEREBY DECLARE MY wholehearted support of the COMMUNITY'S MANIFESTO developed by the citizens of** Mukuru Kwa Rueben, Mukuru Kwa Njenga, Viwandani and Imara Daima Wards of the Embakasi South and Makadara Constituencies**. I further COMMIT to support and work diligently towards the implementation and full realization of the developmental concerns outlined in the COMMUNITY'S MANIFESTO once elected in the office that I seek.**

**Candidate:**

**Signature: ..........................................................................................**

**Date: ..................................................................................................**

**Witness:** Citizen of Mukuru SPA

**Signature: ..........................................................................................**

**Date: ..................................................................................................**

**Witness:** Member of Mukuru SPA Working Group/Committee

**Signature: ..........................................................................................**

**Date: ..................................................................................................**



"It is our hope that our manifesto will act as **an agreement between you, as an aspiring candidate and us the people of Mukuru** and that it will be at the heart of all development programs undertaken in our 4-Wards, for the next five years."



We, the People of Mukuru would like to give special thanks to Ruben Centre and Akiba Mashinani Trust for their support in the development of this Manifesto.

For inquiries: **0778 848 801**